OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULAGA
SHULE YA SEKONDARI CELINA KOMBANI
SLP 100
MAHENGE/ULANGA

Kumb. Na.S.2430/CKSS/HM/2021
Jina mwanafunzi
.....
.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari CELINA KOMBANI kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2021.Aidha uongozi wa shule unachukua fursa hii kukupongeza na kukukaribisha katika jumuiya ya shule Sekondari Celina Kombani

Celina Kombani ni shule ya serikali na ya kutwa na kwa wasichana na wavulana iliyopo umbali wa km 43 kutoka makao makuu ya wilaya

Shule itafunguliwa rasmi kwa muhula wa kwanza tarehe11/01/2021 hivyo utatakiwa kuripoti shuleni kwaajili ya usaili tarehe 09/01/2021, na tarehe 11/01/2021 masomo yataanza rasmi. Pia unapokuja unatakiwa uongozane na mzazi au mlezi kwa ajili ya maelekezo zaidi.

Utakaporipoti shuleni utatakiwa kuwa na vitu vifuatavyo

1. **SALE YA SHULE**
   - **WAVULANA**
     i. **Suruali:** Rangi ya kitambaa **ZAMBARAU NZITO** iliyoshonwa katika maadili yanayokubalika na jamii, iwe na linda, iwe na Pindo chini (TURN UP) na isiwe ya kubana(upana 16 cm). Mshono wake usiwe mfano wa jinsi. Kinyume na hapo suruali hiyo haitakubalika na utalazimika kushona nyingine. Ilikuepuka mpishano wa sare hizo,kabla ya kushona sale wasiliana na uongozi wa shule ili upewe maelekezo ya aina ya kitambaa na namna ya ushonaji.
     ii. **SHATI**: Shati la kitambaa cheupe mikono mifupi lisilobana mwili na liwe na kola
     iii. **VIATU**: Viatu vyeusi vya ngozi napia vya kufunga na kamba na visiwe na kisingino kirefu
     iv. SOKSI: Soksi ndefu nyeupe
   - **WASICHANA**
     i. **SKETI:** Rangi ya **ZAMBARAU NZITO** iliyoshonwa katika maadili yanayokubalika na jamii, mshono wake ni rinda boksi, iwe ndefu hadi chini ya magoti, sketi fupi na zisizo za kitambaa sahihi hazitakubaliwa na utalazimika kushona nyingine. Ili kuepuka mpishano wa sare hizo, kabla ya kushona sale utapaswa kuwasiliana na uongozi wa shule ili kuelekezwa aina ya vitambaa na namna ya ushonaji.
     ii. **BLAUZI/SHATI:** Shati la rangi nyeupe mikono mifupi, lisilobana mwili na ndani ya shati msichana atavaa nguo nyingine. **SHUMIZI/VESTI**
     iii. **VIATU:**Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visiwe na kisigino kirefu
     iv. **SOKSI:** Soksi ndefu nyeupe

NB :

- Kwa wanafunzi wa kiislamu watakaohitaji kuvaa hijabu watavaa hijabu za rangi nyeupe na zisiwe na urembo wa aina yoyote.
- T-Shirt dark blue zenye nembo ya shule zinapatikana kwa utaratibu utakaopewa na shule mara baada ya kuripoti

2. SARE ZA MICHEZO

i. Kwa wanafunzi wa kiume wanatakiwa kuwa na bukta ya bluu, fulana/T-shirt ya dark bluu na raba
ii. Kwa wanafunzi wa kike wanatakiwa kuwa na traki suti ya bluu, T-shirt/fulana ya dark bluu na raba

3. VIFAA ZA MICHEZO

i. Madaftari tisa (9) counter book quire [2 au 3]
ii. Madaftari madogo tisa [9] ya mazoezi
iii. Mkebe wa hisabati [mathematical set]
iv. Peni za bluu au nyeusi, rula, kifutio.
v. Kamusi ya kiingereza [dictionary]
vi. Vifaa vya usafi [ndoo ndogo1, mfagio wa mti, jembe, kwanja]
vii. Faili (1) kwajili ya kuifazia mitihani na mazoezi mbalimbali atayofanya.

4. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa kufuata sheria na taratibu za shule muda wote awapo shuleni na popote alipo nyumbani.

SHERIA NA KANUNI HIZO NI ZIFUATAZO

i. Heshima kwa viongozi , wazazi, wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla
ii. Kuhudhuria katika kila shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
iii. Kushiriki kwa ukamilifu na umakini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
iv. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazo pewa
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo
vi. Usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
viii. Kuvaa sare za shule wakati wote unapo takiwa
ix. Kutunza mali za umma
x. Kuzingatia matumizi ya lugha ya kujifunzia na kufundishia (kiingereza)

5. MAKOSA YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa kuwa mfano bora kwa jamii inayo mzunguka, hivyo ni hamu ya shule kuona kuwa mwanafunzi anakuwa mfano wa kuigwa na jamii ili kusaidia kimaadili na kitaaluma, yafuatayo ni makosa yanayo weza kumfukuzisha au kumsimamisha shule mwanafunzi

a. Wizi

b. Ubakaji
c. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, mfano : bangi, pombe, sigara, milungi, kubeli,cocain n.k
d. Kupiga au kupigana
e. Kuharibu mali za shule kwa makusudi
f. Kupata au kusababisha ujauzito
g. Kudharau bendera ya Taifa
h. Kuoa au kuolewa
i. Kutoa mimba (arbortion)
j. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au wa watu
k. Kukataa adhabu
l. Kuwa na simu ya mkononi

6. Mambo mengine muhimu yanayo paswa kukamilishwa na kuwasirishwa shule ni MEDICAL EXAMINATION FORM ambayo itajazwa na mganga wa hospitali ya serikali na baada ya vipimo fomu hiyo itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara tu utakaapo ripoti shuleni

HEADMASTER
CELINA KOMBANI SEC. SCHOOL
P. O. Box 100
MAHENGE-ULANGA

.....
CHRISTOPHER L. MAPUNDA
MKUU WA SHULE
CELINA KOMBANI SEKONDARI
0714001295/0789839759